

# HATUA ZINAZOFUATA Facilitator Notebook

## Hatua ya 5 | Kuwasikiliza Watoto

© Loom International 2025

LOOM INTERNATIONAL | 2019 | PORTLAND, OR

# HATUA YA 5 MUHTASARI:

Ili watoto waweze kuishi kwa ukamilifu maisha ambayo Mungu amewanuia, fikra zao, mawazo yao, na hadithi zao lazima ziheshimiwe na kuthaminiwa. Watoto huwasiliana nasi kila wakati lakini hatusikilizi kila wakati. Mawasiliano yao huwa si ya maneno kila mara, mara nyingi huwa ya tabia. Kuwasikiliza watoto kunaonyesha kwamba tunaamini wana hadhi na jukumu muhimu la kutekeleza katika ufalme wa Mungu.

## Malengo ya Kujifunza:

Washiriki wata:

- Jifunza umuhimu na faida za kuwasikiliza watoto
- Jifunza kutumia stadi na mitazamo inayotakiwa ili kuwa msikilizaji bora wa watoto na kuwahimiza kuwasiliana
- Jifunza kuwahudumia watoto kwa hadhi na heshima
- Jitoa kuwasikiliza na kuwashirikisha watoto katika maamuzi yanayowahusu watoto

---

## Mpangilio:

I. Kwa nini Usikilize?
II. Nini Hufanyika Wakati Hatusikilizi
III. Jinsi ya Kusikiliza
IV. Utekelezaji – Ni hatua gani utakazochukua?

---

## Maandalizi Kabla ya Kipindi:

Utahitaji kuandaa shughuli zifuatazo kabla ya kipindi hiki. Soma shughuli hiyo na ukusanye vifaa ambavyo unaweza kutumia kuikamilisha shughuli hiyo.



## SHUGHULI YA DARASANI # 1 | WA 86

**Kuta za Matofali Zinazozuia Kusikiliza**
Katika shughuli hii washiriki wataangalia mitazamo na uwongo wanaouamini unaotuzuia kuwasikiliza watoto, kuwaruhusu watoto kuzungumza, na kuwahusisha watoto.

Utahitaji kipande cha karatasi ya upana wa mita 1 kwa wanafunzi kuambatisha "matofali" yao juu yake.

**Maagizo:**

- Katakata karatasi katika vipande vyenye ukubwa wa 'matofali'.
- Acha tofali moja au mawili juu ya dawati la kila mshiriki kabla ya kipindi kuanza.

## SHUGHULI YA DARASANI # 2 | WA 90

**Mtoto Anaweza kusema Msikilizaji Mzuri ni…**
Kabla ya kipindi andika sentensi zifuatazo juu ya vipande vya karatasi vya ukubwa wa kutosha ili washiriki waweze kuviona wakiwa kwenye madawati yao na uviweke kwenye sehemu kadhaa za darasa.

Watoto husema msikilizaji mzuri ni mtu ambaye:

- anakupenda kwa nia safi
- anataka kusikia kile unachosema
- hukuangalia lakini hakukodolei macho
- hukupa kitambaa cha kujipangusa ili ujue ni sawa kulia
- ni mtu halisi na wa kweli
- hakuhukumu bali amekukubali
- hujaribu kuuona ulimwengu kwa mtazamo wako na jinsi ulivyohisi ndani yake
- hukaa nawe muda wa kutosha ili uhisi yuko nawe
- husubiri kuambiwa 'aingie' kwenye mawazo na hisia zako
- hukuruhusu ukae ndani ya kasri lako ikiwa hauko tayari kutoka nje

## SHUGHULI YA DARASANI # 3 | WA 92

**Maigizo Mafupi ya Jinsi ya Kusikiliza**
Kabla ya kipindi chako, amua ni jinsi gani utawaeleza washiriki wako kuhusu kusikiliza kimyakimya, kwa matendo na kwa kuonyesha huruma. Inapendekezwa utumie maigizo mafupi katika kipindi hiki lakini hii inahitaji uwe na watu wengine zaidi.

## SHUGHULI YA DARASANI # 4 | WA 97

**Njia zisizotisha za kuanza kuzungumza**
Kwa shughuli hii, utahitaji vifurushi vya pipi zenye rangi nyingi.

## SHUGHULI YA DARASANI # 5 | WA 98

**Ongea na Ucheze**
Kwa shughuli hii, utahitaji meza iliyojaa vitu mbalimbali vya kuchezea: wanyama wadogo, magari, wanasesere, mipira, udongo wa kuchezea, matofali madogo na vitu vingine vya kuchezea unavyoweza kukusanya.

## SHUGHULI YA DARASANI # 6 | WA 98

**Wakati Uliopita, wa Sasa, Ujao**
Ili kuwasaidia washiriki kuelewa wanachotarajiwa kufanya katika shughuli hii, itakuwa vyema ikiwa msimamizi atataja mfano kutoka kwa maisha yake.

Kwa shughuli hii, utahitaji karatasi kubwa (11 x 17 au A3) na kalamu za rangi au penseli za rangi.

---



### Kiambatisho

1. Wakati uliopita, sasa, yajayo

# HATUA ZINAZOFUATA - HATUA YA 5




## Mbona Usikilize?


Kwanza - fikiria juu ya kitu fulani kilichokufanya utabasamu, kilichokupendeza au kilichokufurahisha katika wiki chache zilizopita...

**Maagizo:**


- Waambie washiriki wafikirie juu ya kitu kilichowafanya watabasamu katika wiki 2 zilizopita na wamgeukie jirani yao na washiriki nao hadithi ya dakika 2 kuhusu tukio hilo.
- Baada ya kumaliza, waulize maswali yafuatayo.

**Uliza:**

- Je, ulihisi kwamba mwenzako alikuwa anasikiliza?
- Ulijuaje alikuwa anasikiliza kwa kweli?
- Je, ilikuwa muhimu kwako kwamba alisikiliza? Kwa nini?
- Ulihisi umeheshimiwa?





Kiini cha kusudi la kuwaumba wanadamu na mazingira ya duniani ni thamani na furaha ya Utatu kuwa na uhusiano na mawasiliano. Watu waliumbwa na hitaji la msingi la uhusiano & mawasiliano.




Ni tabia ya kiungu kuwapa watu muda na heshima na kuwasikiliza. Pia ni tabia ya kiungu kutarajia kusikilizwa.

Kila mwanadamu aliumbwa asikilizwe na asikilize. Hiyo ndiyo njia pekee ya sisi kupata uzima tele ambao Mungu alinuia tuwe nao.

## CLASS MAJADILIANO





Uliza kundi lote maswali haya - Subiri watu wachache watoe majibu mafupi kwa swali 1 au maswali haya yote nawe ukiyakubali majibu yao.

**Je, mtu huhisi vipi anapokosa kusikilizwa -**
Kama mtu mzima, wewe huhisi vipi unapokosa kusikilizwa? Na rafiki yako, mfanyakazi mwenzako, mwajiri wako, watoto wako?

- o Ukiwa mtoto, je, unakumbuka wakati ambao hukusikilizwa? Ulihisi vipi?
- o Ukiwa mtoto, je, uliacha kuongea?

Tunavyohisi ndani yetu wakati tunajua hatujasikilizwa ni hisia sahihi kwa sababu tuliumbwa kusikilizwa.




### Kwa nini Usikilize?

Hitaji la watoto kusikilizwa ni muhimu zaidi. Ni jambo muhimu katika ukuaji wa hisia zao, ubongo wao, kuingiliana kijamii na kuhisi wana thamani ulimwenguni. Kama tulivyojifunza katika vipindi vya awali, ili tuweze kukuza akili, mwili na roho nzuri, mtu fulani anahitaji kututendea mambo kwa hadhi na heshima na kutusikiliza katika hatua mbalimbali za ukuaji wetu. Kusikilizwa na kujifunza kusikiliza huathiri hali njema ya mtoto kiakili, kijamii, kihisia na kiroho.

Huwa tunawasikiliza watoto kwa sababu ili waweze kuchukua kitambulisho na maisha ambayo Mungu amenuia kwao, mawazo yao, maoni na hadithi zao lazima zikubaliwe na kuitikiwa.




Kumbuka Kweli ya Mfumo wa Biblia # 1 — Mungu humuumba kila mtu kama mtoto aliye na hadhi.

Watoto wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu wakiwa na thamani sawa na watu wazima lakini wana hitaji kubwa zaidi la ulinzi na malezi.

Hadhi, thamani ni maudhui yanayoendelea katika nia za Mungu kwa watoto.

Hadhi haihusu uwezo, kipawa, utamaduni, hali za kijamii, au hali ya uchumi. Mtu hupewa na Mungu.